

MIMI NI MTOTO WA MFALME

Kwa sababu Yesu Kristo ni nani, na

Kwa sababu ni mwokozi wangu na Mungu wangu:

Mimi ni mtoto wa Mfalme wa wafalme na Mungu wa miungu,
nimekaa na Kristo kwenye ufalme wa mbinguni. Nimechaguliwa, nimekubaliwa,
na nimejumuishwa – ni mwanachama wa mbinguni na mtu wa nyumbani mwa Mungu.

Ninapendwa na Mungu kwa halizote na bila kubadilika.

Mimi ni wake, niliyenunuliwa nae kwa damu ya Yesu ya thamani.

Nina Maisha ya umilele na nitaokolewa wakati wa unyakuo – nimehakikishiwa!

Mimi ni mkristo. Si watofauti tu kulingana na ninayo yafanya.

Utambulisho wangu umebadilika. Nimebadilika.

Kila kitu kime kuwa na utambulisho mpya.

Mimi ni sehemu ambayo Mungu anaishi ndani yangu kupitia Roho wake.

Ninaweza kumpata wakati wowote, mahali popote, kwa sababu yoyote.

Mimi ni uumbaji wa Mungu – kazi ya mikono yake. Niliumbwa nae na kwa ajili yake hivyo
mimi nilivyo na ninachofanya kinaumuhimu sana.

Kiroho ninaishi. Nmewekwa huru na woga wa kifo

Nimepewa maisha kuishi na kufurahia kabisa

Nimesamehewa – kabisa, kwa ukamilifu, na uhakika kabisa.

Nimekombinelewa kwenye muunganiko wa giza

Na nimeletwa kwenye Ufalme wa Nuru – Ufalme wa mwana wake.

Nimekombinelewa kwenye adhabu ya dhambi na nguvu ya dbambi

Mimi ni adui wa shetani na nipo kwenye vita na nguvu za kiroho za shetani

Lakini mkuu ni yeye yule aliye ndani yangu kuliko yeye aliye duniani.

Kama Mungu yupo kwa ajili yangu, haijalishi nani au nini kinasimama kinyume na mimi,
kwasababu hakuna kitu wala mtu atakayenitenga na upendo wa Kristo –

siyo maumivi, hasara, matatizo au uharibifu;

siyo matezo, adha, magumu au hatari,

siyo kutelekezwa, kukataliwa, mazoea kupiliza kwenye vitu au hamu zozote;

siyo matamano, vyakula, jinsia au mahusiano;

siyo maisha au kifo, Malaika au mapepo;

siyo yakale, yasasa au yajayo;

siyo nguvu, siyo mtu, siyo mahali, siyo kitu chochote kwenye uumbaji wote;

siyo hata shetani anayeweza kunizuia.

Niko mikononi mwa Yesu, mikononi mwa Mungu, na hakuna chochote

Na hakuna yeyote anayeweza kunitoa mikononi mwa Mungu.

Sltamuogopa shetani maana Mungu yupo Pamoja na mimi, na

Ameniahidi kutokuniacha wala kunitenga mimi.

Uwepo wa Mungu uko na mimi kila mahali ninapokwenda -

mpaka vimo vya mbinguni,

kupitia bonde la uvuli,

mpaka miisho ya dunia – milele na wakati wote.

(Ufun.1:8, Yoh 1:12)

(Efes.2:6, 1Petro2:9)

(Yoh14:1-6, Waef2:19)

(War.5:6-8, 1Yoh4:10)

(1Petro2:9, 1Kor 6:19)

(1Yoh 5:11-13, Yoh 3:16)

(War. 5:9, Efes 1:13-14)

(1Petrp 4:16)

(IIKor.5:17, Gal 2:20)

(Efes. 2:22, 1Kor 6:19)

(Efes. 2:18, Filp. 4:6-7)

(Zab. 138, Efes. 2:10)

(Kor. 1:16, Gal.6:7-9)

(War.6:8-11, Ebr. 2:14-15)

(Yoh.10:10)

(1Yoh.1:9, Zab.103:8-13)

(Kol. 1:13)

(War. 6:16-23, Gal.5:1)

(1Petro 5:8, Efes.6:12)

(1Yoh. 4:4)

(War. 8:31, Efes.1:18-23)

(War. 8:35-39)

(Kol. 2:15)

(Yoh 10:27-28)

(Zab23:4, IITim. 1:7)

(Ebr. 13:5)

(Zab. 139:7)

(Math. 28:19-20)

Mimi ni mtoto wa Mfalme na nimechangua siku hii ya leo kuishi kama mmojawapo.